



Association Internationale Aphasie (AIA)

Afasia ni **tata ya lugha**

Watu ambao wanaugua kutokana na afasia huwa na shida ya **kuongea, kuelewa, kusoma, kuandika na kufanya hesabu.**

Chanzo cha afasia kwa kawaida huwa **madhara ya ubongo.** Katika kesi nyingi hii huwa ni **kupindwa na mshipa**, lakini pia **ajali au kidonda** inaweza kusababisha afasia.



Mtu huugua kutokana na kupindwa na mshipa wakati **mzunguko wa damu** katika ubongo unatatizwa kwa **ghafla.**

Hii inaweza kutokana na mambo mawili: mshipa wa damu unaweza **kuzibika** au mshipa unaweza kuanza **kuvuja**

Kuzibika:

Kwa ajili ya **kunenepa kwa ukuta wa mshipa** (thrombosis) au kwa maana ya **damu kuganda** (embolism) mshipa unaweza kuzibika.

Hii inaitwa *cerebral infarction*



Kuvuja:

Sehemu **nyepesi** inaweza kuundika ndani ya mshipa (aneurysm); na sehemu hiyo inaweza **kupapa** na kuanza **kuvuja** au **kupasuka.**

Hii inaitwa *cerebral heamorrhage*



Madaktari kwa kawaida huiita kupindwa na mshipa CVA; **Cerebral Vascular Accident**

Lugha huwa na sehemu muhimu katika maisha yetu ya kila siku.

Tunazungumza na watu wengine, **tunasoma** magazeti, **tunafanya kazi** na **tunaelimika**.

Pia tunatumia lugha kutunga **fikira** zetu na kutoa **mipango** za siku za usoni.

Watu ambao wanaugua kutokana na afasia wanaweza kuwa na **shida** katika mambo kadhaa ambayo kabla ya afasia yalikuwa ya kawaida:

- Kuzungumza
- Kuongea na wenzio au katika mazingira yenye kelele
- Kusoma kitabu, gazeti au jarida au hata alama za bara barani.
- Kuelewa na kusema vichekesho
- Kuelewa vipindi kwenye runinda au redio
- Kuandika barua au kujaza fomu
- Kupiga simu
- Kufanya hesabu, kukumbuka nambari au kukabiliana na pesa
- Kutaja jina zao au majina ya wanafamilia zao



Watu wanaougua kutokana afasia huwa na shida katika lugha, lakini **sio wenda wazimu!**

Watu wengi ambao wanaugua kutokana na afasia hupata kuwa maisha yao **yamebadilika** sana.

Mambo ambayo yalikuwa rahisi mwanzoni, yanachukua **muda na jitihada** nyingi.

Watu wengi ambao wanaugua kutokana na afasia **hutokuwa na udhabiti** na kuwa na **kuhangaika** kuhusu jinsi ya kuendelea na maisha.

Msaada na himili kutokana na mazingara yao ni muhimu sana.

Kukutana na watu wengine ambao wanaugua kutokana na afasia pia husaidia.

Watu wanaugua kutokana na afasia **huelewana bila kutumia maneno**.

Wewe unaweza kufanya nini?

- **Waambie watu** kuwa unaugua kutokana na afasia
- Vaa **cheti ndogo**, ambayo inaonyesha afasia ni nini
- Bainisha kile unachomaanisha kwa kutumia **gesture***, **michoro**, **maandishi**, au **onyeshea kidole** kama kusema hakuendi vyema
- Omba **msaada** kwa familia
- **Tangulia kwa kupanga**, andaa gumzo kwenye fikira zako au kwenye karatasi.
- Gawa hangaiko zako na wengine; usihangaike peke yako.



gesture



michoro



maandishi



onyeshea kidole